**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

## 112 SANAA ZA UBUNIFU NA MICHEZO

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO


DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI........ 1

2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA........ 1

3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ........ 1

3.1 SEHEMU A: MASWALI MCHANGANYIKO ........ 1

3.1.1 Swali la 1: Kuchagua jawabu lililosahihi ........ 1

3.1.2 Swali la 2: Kuchagua jawabu Sahihi kutoka Kifungu A na Kifungu B........ 4

3.1.3 Swali la 3: Kuandika Kweli au si Kweli........ 5

3.1.3 Swali la 4: Kujaza Mapengo........ 7

3.2 SEHEMU B: MASWALI MCHANGANYIKO........ 9

3.2.1 Swali la 5: Sanaa za lugha ........ 9

3.2.2 Swali la 6: Uchongaji ........ 11

3.2.3 Swali la 7: Ubunifu........ 12

3.2.4 Swali la 8: Kuogolea ........ 14

3.2.5 Swali la 9: Afya katika Michezo........ 16

3.3 SEHEMU C: MASWALI YA KUELEZEA KWA UREFU........ 19

3.3.1 Swali la 10: Unyanyasaji wa Kijinsia........ 19

3.3.2 Swali la 11:Afya katika Michezo........ 21

3.3.3 Swali la 12: Ubunifu........ 22

4.0 HITIMISHO ........ 23

5.0 MAPENDEKEZO........ 23

VIAMBATANISHO ........ 24

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Kwanza katika somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa Kuingilia Kidatu cha Kwanza ni kigezo cha miaka mitatu ya Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi hupimwa ni kwa kiasi gani wameweza kufahamu masomo yao ya Darasa la tano (5) hadi la saba (7). Hivyo, mtihani huu ni maandalizi tosha kwa ajili ya Elimu ya Sekondari ya Awali.

Uchambuzi uliyowasilishwa katika ripoti hii, unakusudia kuonesha sababu mbalimbali juu ya majibu ya Watahiniwa katika Somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo. Ripoti inabainisha sababu tofauti zilizopelekea watahiniwa kujibu vizuri au vibaya. Miongoni mwa sababu za watahiniwa kufanya vizuri ni ufahamu mzuri wa mada zilizotahiniwa na uelewa mzuri wa maswali na kile walichoulizwa.

Aidha, watahiniwa walijibu vibaya kwa baadhi ya maswali kwa sababu zifuatazo, ufahamu mdogo wa mada walizofundishwa, uwelewa mdogo hasa katika maswali ya kuelezea na kushindwa kukumbuka dhana mbalimbali walizofundishwa.

Kwa kuendelea zaidi, uchamnbuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia jadweli ambazo zimebainishwa kwa rangi tofauti na zinaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, ni Imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa Elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo katika Mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar na la Taifa.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha taarifa hii.

**Dkt. RASHID .A. MUKKI**



**MKURUGENZI**
**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**
**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa kuingia Kidato cha Kwanza kwa somo la Sanaa za Ubunifu na Michezo Mwaka 2022. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Zanzibar wa mwaka 2009 na 2022 na kufuata muundo wa mtihani wa Darasa la Saba wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2022.

Mtihani wa Sanaa za Ubunifu na Michezo ulikuwa na maswali kumi na mbili (12) ambayo yalikuwa katika mgawanyiko wa sehemu A B na C. Sehemu A na B zilikuwa ni za lazima ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4) na sehemu B ilikuwa na maswali matano (5) na Sehemu C ilikuwa na maswala matatu (3) ambapo watahiniwa walitakiwa wachague swali moja (1).

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **4,521** sawa na asilimia **11.08** ya watahiniwa **40,790** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 20, wastani 21 hadi 60 na vizuri 61 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia jadweli kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B na C. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa.

### 3.1 SEHEMU A: MASWALI MCHANGANYIKO

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) kutoka katika mada mchanganyiko zikiwemo "Kuogelea, huduma ya kwanza katika michezo, ubunifu, mapishi, ujasiriamali na udhalilishaji. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote manne (4) ambapo swali la kwanza, la tatu na la nne yalikuwa na alama kumi (10) kwa kila moja na swali la pili lilikuwa na alama tano (5). Hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama thelathini na tano (35).

#### 3.1.1 Swali la 1: Kuchagua jawabu lililosahihi

Swali hili limetoka kwenye mada mchanganyiko ambazo ni Huduma ya kwanza katika Michezo, Ubunifu, Afya katika Michezo, Uchongaji na Sanaa za Lugha na Maigizo. mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi na kuandika herufi ya jawabu katika jadweli iliyotayarishwa. Swali hili lilikuwa na vipengele kumi (10) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama moja (1) na kufanya swali zima kuwa na alama 10.

**Uchambuzi wa Swali la kwanza (i)**

Ufuatao ni uchambuzi wa kila kipengele katika swali la kwanza (1).

**Kipengele nambari (i)**

Kipengele hiki kilimtaka Mtahiniwa kuchagua mchezo wa riadha kutoka katika orodha ya michezo mbali mbali. Swali lilikuwa na vichachawizi kama vifuatavyo:

A: Kukimbia, kuruka na kuogelea; B: Kukimbia, kurusha na kuruka; C: Kukimbia, kupika na kurusha; D: Kurusha, kuogelea na kupika

Kipengele hiki kilikuwa na maelezo haya '*uchongaji ni njia mpja wapo itakayomsaidia mtu kuweza'* Mtahiniwa alitakiwa kuainisha faida ya uchongaji. Vifungu vya maneno vilikuwa kama ifuatavyo:

A: Kupoteza mda; B: Kujipatia kipato;

C: kusaidia watu kazi zao; D: kufanya matembezi

**Kipengele nambari (iii),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuainisha zana zinazohitajika katika upishi wa ugali, kati ya vifungu vilivyoorodhshwa, vilikuwa kama ifuatavyo:

A: maji, moto, sufuria, unga na mwiko; B; maji, moto, unga, sufuria, samli na kijiko;

C: maji, mwiko, kopo, chumvi na unga; D: mwiko, unga, moto, kopo na kijiko.

**Kipengele nambari (vi),**

Mtahiniwa alitakiwa kubaini msingi wa ujasiriamali kutoka kwenye vifungu vifuatavyo:

A: mfanya biashara; B: mjasiriamali; C: mtaji; D: usafiri

**Kipengele nambari (v),**

Mtahiniwa alitakiwa kuainisha vifaa visivyokuwa vya uokozi. Vichachawizi vilikuwa kama ifuatavyo:

A: boya la uokozi; B: chuma cha uokozi;

C: koti la uokozi; D: rafti ya kuokoa maisha.

**Kipengele nambari (vi),**

Mtahiniwa alitakiwa kuchagua miongomi mwa aina za ngoma zisizo za asili, kutoka kwenye orodha waliyopewa kama ifuatavyo:

A: Kidumbaki; B: msewe; C: msondo D: Zenji fleva.

**Kipengele nambari (vii),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kubainisha sifa za mashairi ili kuitambulisha kazi ya ushairi. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jawabu katika orodha ifuatavyo:

A: Kutumia kipaza sauti; B: Kutumia lugha ya mkato;

C: Kutumia ngoma; D: Kutumia vinanda.

**Kipengele nambari (viii),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuainisha utanzu wa fasihi ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua kwenye orodha ifuatyao:

A: ngoma; B: Riadha; C: Shairi; na D: tamthilia

**Kipengele nambari (ix),**

Katika kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kubainisha aina za udhalilishaji uliooneshwa kutpitia kwenye igizo, mtahiniwa alitakiwa kuchagua kutoka kwenye orodha ifuatayo:A: wizi; B: rushwa; C: udhalilishaji; D: burudani.

.**Kipengele nambari (x),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuainisha maana ya kujitambua, kutoka kwenye orodha ifuatayo:

A: kuwatambua wengine katika jamii; B: kuwafahamu wengine katika jamii;

C: kujitambua mwenyewe na jamii husika; na D: kutambuana katika jamii.

Kwa ujumla swali hili lililenga kuwapima watahiniwa ufahamu kuhusiana na mada tofauti kulingana na maswali yalivyoilizwa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,513** sawa na asilimia **99.82** na watahiniwa **8** sawa na asilimia **0.18** hawakujibu swali husika. Takwimu za ufaulu wa wanafunzi zinaonesha katika jadweli linalofuata hapo chini.


**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 226 | 5.01 | 847 | 18.77 | 3,440 | 76.22 | 4,287 | 94.99 |

Takwimu za Jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **76.22** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri kwa asilimia **94.99.**

Aidha, watahiniwa **226** sawa na asilimia **5.01** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **1.1.**


**Kielelezo 1.1: Kielelezo Kibaya**




Kielelezo **1.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye hakuweza kupata alama kwa sababu mtahiniwa amechagua jawabu zisizo sahihi katika vipengele vyote vya swali hili. Kwa mfano, kipengele cha (iii), jawabu sahihi ni ‘’A’’ ambayo ni (maji, moto, sufuria, unga na mwiko) lakini mtahiniwa amechagua herufi ‘’B’’ ambayo sio sahihi. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na ufahamu na uelewa juu ya kile alichoulizwa.

Aidha, watahiniwa **3,440** sawa na asilimia **76.22** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **1.2**

**Kielelezo 1.2: Kielelezo Kizuri**




Kielezo nambari 1.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika, na ameweza kupata alama kamili ya swali hili. Kwa mfano katika kipengele cha **(iv)** mtahiniwa aliweza kuchagua

‘C’ kuwa ni moja kati ya misingi ya ujasiriamali. Hii imepelekea mtahiniwa kupata alama kamili katika swali nambari moja (1) lenye alama 10.

**3.1.2 Swali la 2: Kuchagua jawabu Sahihi kutoka Kifungu A na Kifungu B**

Swali hili lilikuwa la kuoanisha ambalo lilikuwa na vipengele 5 na kila kipengele cha swali hili lina alama moja (1) na kufanya swali zima kuwa na alama tano (5). Ambapo mtahiniwa alitakiwa kuoanisha maelezo kutoka kifungu A na jibu sahihi kutoka kifungu B.

Swali hili lilitokana na mada ya ‘‘Huduma ya kwanza katika michezo na Afya katika Michezo’’.

**Uchambuzi wa swali nambari 2**

Ufuatao ni uchambuzi wa kila kipengele katika swali nambari **2**

**Kipengele nambari (i),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuoanisha dalili na ishara za kuvunjika. ambapo jibu sahihi lilikuwa ni (E) maumivu makali na uvimbe.

**Kipengele nambari (ii)**

Mtahiniwa alitakiwa kuoanisha hatua muhimu ya utoaji wa huduma ya kwanza ambapo jawabu ilikuwa ni ‘A’ hakikisha usalama wako kwanza.

**Kipengele nambari (iii),**

Katika kipengele cha tatu (iii)

Mtahiniwa alitakiwa kuoanisha dalili ya kupoteza maji na chumvi chumvi mwilini. Jawabu sahihi ilikuwa ni ‘D’ kukakamaa kwa misuli

**Kipengele nambari (iv),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuoanisha faida ya kula chakula bora chenye afya. Ambapo jawabu ilikuwa ‘B’ kuimarisha kinga ya mwili.

**Kipengele nambari (v),**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuoanisha sababu za uvunjifu wa viungo vya mwili wa mwanadamu. Jawabu sahihi ilikuwa ni ‘A’ ukosefu wa vitamin A.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,518** sawa na asilimia **99.93** na watahiniwa **3 s**awa na asilimia **0.07** hawakujibu swali husika. Takwimu ya ufaulu wa wanafunzi unaoneshwa kwenye jadweli **1b** hapo chini.

**Jadweli nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0-1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 - 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 560 | 12.40 | 1364 | 30.19 | 2,594 | 57.41 | 3958 | 87.60 |

Takwimu za Jadweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **57.41** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri hivyo ufaulu wa jumla ni mzuri wa asilimia **87.60.**

Aidha, watahiniwa **560** sawa na asilimia **12.40** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **2.1.**

**Kielelzo kibaya 2.1**

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| B | G | A | C | D |

Kielelezo **2.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vibaya. Kwa mfano katika kipengele (i) jawabu sahihi ilikuwa ni 'E' maumivu makali na uvimbe, lakini mtahiniwa alichagua 'B' ambayo sio jawabu sahihi. Hii ni kutokana na maarifa na ujuzi mdogo aliokuwa nao, pia hakufahamu matakwa ya swali husika.

Kwa upande mwengine, watahiniwa **2,594** sawa na asilimia **57.41** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **2.2**

**Kielelezo 2.2: Kielelezo Kizuri**

JAWABU

| i. | ii. | iii. | iv. | v. |
|---|---|---|---|---|
| E | A | D | B | G |

Kielelezo 2.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwelewa wa kutosha juu ya swali aliloulizwa na kupelekea kuandika majibu kwa usahihi.

### 3.1.3 Swali la 3: Kuandika Kweli au Si Kweli

Swali hili lilitolewa katika mada ya ''Afya katika Michezo, Ubunifu na Ujasiriamali, Kuogolea na Sanaa za Lugha.

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuandika **kweli** kwa maelezo yaliyo sahihi au **si kweli** kwa maelezo yasiyo sahihi. Swali hili lilikuwa na vipengele 10 na kila kipengele kilikuwa na alama moja (1) na kufanya jumla ya alama kumi (10).

**Uchambuzi wa swali nambari 3**

Ufuatao ni uchambuzi wa kila kipengele katika swali nambari 3.

**Katika kipengele nambari (i),**

Kufanya mazoezi bila ya kupumzika hupelekea kushuka kwa kiwango cha utendaji wa mazoezi kwa mwanamichezo.

**Kipengele nambari (ii)**

Pilipili boga, keroti na iliki ni viambaupishi vinavyotumika kupika muhogo.

**Kipengele nambari (iii)**

Vigogo hutumika kutengezea kinu na mchi

**Kipengele namba (iv)**

Masoko si nyenzo muhimu sana kwa mjasiria mali.

**Kipengele namba (v)**

Kuogelea kimgongo mgongo humtaka muogeleaji kupiga miguu kama chura.

**Kipengele nambari (vii)**

Kuburudisha wahusika na hadhira ni moja ya ubunifu wa maigizo.

**Kipengele nambari (viii)**

Mashairi ni kipande cha maandishi kilichopangwa kwa utaratibu maalumu.

**Kipengele nambari (ix)**

Matayarisho y jukwaa katika igizo hayahitaji ubunifu wa mandhari.

**Kipengele nambari (x)**

Vyakula vya protini huliwa na wanamichezo kwa wingi katika kipindi cha mashindano.

Kwa ujumla Swali hili lilikusudia kumpima mtahiniwa ufahamu wake kutokana na dhana mbali mbali zinazotumika katika mada husika.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,511** sawa na asilimia **99.78** na watahiniwa **10 s**awa na asilimia **0.22** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 1c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 106 | 2.35 | 667 | 14.79 | 3,738 | 82.86 | 4,405 | 97.65 |

Takwimu za Jadweli nambari **1c** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **82.86** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **97.65**

Aidha, watahiniwa **106** sawa na asilimia **2.35** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.


**Kielelzo kibaya 3.1**




Kielelezo **3.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya kwenye swali hili. Kwa mfano katika kipengele cha tatu (iii) ‘‘Vigogo hutumika kutengezea kinu na mchi’’,mtahiniwa alitakiwa aandike ‘‘kweli’’ ambalo ndilo jibu sahihi badala yake aliandika ‘‘sikweli’’. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa juu ya swali husika na kupelekea kufanya vibaya swali hili kama inavyoonesha kwenye kielelezo **3.1**.

Aidha, watahiniwa **3,738** sawa na asilimia **82.86** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavythibitisha katika kielelezo nambari **3.2**

**Kielelezo kizuri 3.2**


JAWABU

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kweli | Sikweli | Kweli | Si Kweli | Kweli | Kweli | Kweli | Kweli | Sikweli | Kweli |

Ukurasa wa 4 kati ya 9

Kielelezo 3.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwelewa wa kutosha juu ya swali aliloulizwa na kupelekea kuandika majibu kwa usahihi.

**3.1.3 Swali la 4: Kujaza Mapengo**

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchagua jawabu sahihi na kujaza katika nafasi zilizo wazi. Swali hili lilikuwa na vipengele 5 na kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2) hivyo kufanya jumla ya alama kumi (10). Swali hili limetokana na mada zifuatazo ‘‘Ujasiriamali, Ubunifu na Huduma ya kwanza.’’

**Uchambuzi wa swali nambari 4**

Ufuatao ni uchambuzi wa kila kipengele katika swali nambari.

**Katika kipengele nambari (i),**

Katika swali hili mtahiniwa aliliulizwa ‘Mjasiria mali ni mtu aneweza kuona ________________________ mbali mbali.’

**Kipengele cha (ii),**

Mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi tupu kwenye kifungu cha maneno haya ‘Unga wa maandazi ni lazima ukandwe hadi ________________________________ ili kufanya maanfdazi yawe laini.

**Kipengele cha (iii)**

Katika kipengele hiki mtahiniwa aliulizwa ‘kifaa hupakwa ____________________ baada ya kumaliza kuchongwa ili kivutie’.

**Kipengele cha (iv)**

Mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi kifungu cha maneno ikuatacho: ‘kwenye sekta ya bahari ____________________ ni paumbele cha kwanza’

**Kipengele cha (v)**

Kipengele hiki kiliuliza ‘Msaada wa haraka anapopewa alieumia au kupata jeraha kabla ya kufikishwa hospitali unaitwa _____________________________.’

Kwa ujumla swali hili limelenga kuwapima wanafunzi uwelewa kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika mada mchanganyiko.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,518** sawa na asilimia **99.93** na watahiniwa **3** sawa na asilimia **0.07** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 1d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 0 - 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 345 | 7.64 | 576 | 12.75 | 3,597 | 79.61 | 4,173 | 92.36 |

Takwimu za Jadweli nambari **1d** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **79.61** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **92.36**

Aidha, watahiniwa **345** sawa na asilimia **7.64** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **4.1.**

**Kielelzo kibaya 4.1**




4. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuchagua jibu sahihi.
   i. Mjasiriamali ni mtu anaeweza kuona Vanish mbali mbali.
   ii. Unga wa maandazi ni lazima ukandwe hadi fursa ili kufanya maandazi yawe laini.
   iii. Kifaa hupakwa Uumuke baada ya kumaliza kuchongwa ili kivutie.
   iv. Kwenye sekta ya bahari huduma ya ni kipaumbele cha kwanza.
   Msaada wa haraka anaopewa alieumia au kupata jeraha kabla ya kufikishwa hospitali unaitwa ya kwanza

Vanish, fursa, uumuke, huduma ya kwanza, ulainike, hospitali, usalama.

Kielelezo **4.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya swali hili. Mfano katika kipengele cha (i) mtahiniwa aliandika ''vanish'' badala ya kuanika 'fursa' ambalo ndio jibu sahihi. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na uwelewa wa kutosha katika swali aliloulizwa.

Kwa upande mwengine watahiniwa **3,597** sawa na asilimia **79.61** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari 4**.2.**

**Kielelzo kizuri 4.2**



4. Jaza nafasi zilizowazi kwa kuchagua jibu sahihi.
   i. Mjasiriamali ni mtu anaeweza kuona fursa mbali mbali
   ii. Unga wa maandazi ni lazima ukandwe hadi ulainike ili kufanya maandazi yawe laini.
   iii. Kifaa hupakwa vanish baada ya kumaliza kuchongwa ili kivutie.
   iv. Kwenye sekta ya bahari Usalama ni kipaumbele cha kwanza.
   v. Msaada wa haraka anaopewa alieumia au kupata jeraha kabla ya kufikishwa hospitali unaitwa Huduma ya kwanza

Vanish, fursa, uumuke, huduma ya kwanza, ulainike, hospitali, usalama.

Kielelezo **4.2** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na uwelewa wa kutosha juu ya swali aliloulizwa na kupelekea kuchagua majibu katika kisanduku kwa usahihi.

### 3.2 SEHEMU B: MASWALI MCHANGANYIKO

Sehemu hii ilikuwa na maswali matano (5) ambapo kila swali lilikuwa na alama tisa (9) hivyo katika sehemu hii inafanya jumla ya alama zote kuwa ni arobaini na tano (45).

#### 3.2.1 Swali la 5: Sanaa za Lugha

Swali hili linatokana na mada ya 'Sanaa za Lugha', swali hili lilikuwa na vipengele vitatu. kipengele (a, b na c) kila kipengele kilikuwa na alama tatu (3) na kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama tisa (9).

Kipengele (a)

kipengele hiki kililenga kumpima mtahiniwa kuelezea maana ya tamthilia'.

Kipengele (b)

Katika kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kutaja aina tatu (3) za tamthilia

Kipengele ( c)

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kuandika njia tatu (3) za uandaaji wa tamthilia.

Kwa ujumla swali hili lililenga kuwapima watahiniwa juu ya ufahamu wao juu ya dhana ya tamthilia.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,406** sawa na asilimia **97.46** na watahiniwa **115** **s**awa na asilimia **2.54** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,468 | 33.32 | 1207 | 27.40 | 1,731 | 39.28 | 2,938 | 66.68 |

Takwimu za Jadweli nambari **2a** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **39.28** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **66.68.**

Aidha, watahiniwa **1,468** sawa na asilimia **33.32** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya dhana ya tamthilia kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **5.1**.

**Kielelzo kibaya 5.1**


5. a. Elezea maana ya tamthilia.

Tamthilia ni Utungo Uleambo kuwa kutanisha watu wa aina 1 nne au mbalimbali kupita Igizo.

Taja aina tatu (3) za tamthilia.

Tathlitha

Talbia

Talthitha

Andika njia tatu (3) za uandaaji wa tamthilia.

Isomeke. Vizuri

Kuwa na wahusika wanne tu. wasizidi wengine


Imbike na kuleta kituchamaara

Itumie lugha moja tu ya kiswahili.

Kielelezo **5.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya katika swali hili. Mfano katika kipengele (a) 'Elezea maana ya tamthilia' mtahiniwa hakuweza kueleza kama swali livyotaka. Hii inaonesha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na uwelewa wa kutosha katika swali aliloulizwa.

Aidha, watahiniwa **1,731** sawa na asilimia **39.28** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu maana na dhana ya tamthilia kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari 5**.2**

**Kielelzo kizuri 5.2**


5. a. Elezea maana ya tamthilia.

Tamthilia ni fasihi andishi inayowasilishwa kwa njia ya mazungumzo na matendo jukwaani.

b. Taja aina tatu (3) za tamthilia.

i) Tamthilia chesh

ii) Tamthilia tanzia

iii) Tamthilia melodrama.

c. Andika njia tatu (3) za uandaaji wa tamthilia.

i) Kuandaa aina ya tamthilia

ii) Kuandaa wahusika ndani ya tamthilia hiyo

iii) Lazima tamthilia itakayo andaliwa iwe na jina la ke maalumu.

Kielelezo **5.2** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na ufahamu mzuri juu ya swali aliloulizwa na kupelekea kujibu swali kwa usahihi kama lilivyotaka.

### 3.2.2 Swali la 6: Uchongaji

Swali hili linatokana na mada ya ‘Uchongaji’, swali hili lilikuwa na vipengele viwili, kipengele (a na b) kipengele (a) kilikuwa na alama tatu (3), na kipengele (b) kilikuwa na alama sita (6), hivyo swali zima lilikuwa na alama tisa (9).

Swali hili lililenga kumpima mtahiniwa juu ya dhana nzima katiaka mada ya ‘Uchongaji’.

**Kipengele (a)**

Kipengele hiki kimtaka mtahiniwa aeleze maana ya kuchonga.

**Kipengele (b)**

Katika kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kutaja vifaa sita (6) vinavyohitajika wakati wa kuchonga pamoja na matumizi yake.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,485** sawa na asilimia **99.20** na watahiniwa **36** **s**awa na asilimia **0.80** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 641 | 1,4.30 | 1,295 | 28.87 | 2,549 | 56.83 | 3,844 | 85.70 |

Takwimu za Jadweli nambari **2b** zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **56.83** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **85.70**

Aidha, watahiniwa **641** sawa na asilimia **14.30** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya maana na dhana nzima ya uchongaji kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **6.1**.

**Kielelzo kibaya 6.1**


a. Elezea maana ya kuchonga.

Ni ile hali ambapo mwanadamu huonesha Istara zake kuwa kupitia mambo tofauti ya kubuni ~~kama vile~~ ~~kalas~~ ya uchongaji.

Ukurasa wa 5 kati ya 9


b. Taja vifaa sita (6) vinavyohitajika wakati wa kuchonga pamoja na matumzi yake.

| Na. | KIFAA | MATUMIZI |
|---|---|---|
| i. | Patasi | Vifaa vya kusungua |
| ii. | Msumeno | Niule anachongea |
| iii. | BisiBisi | Niile ya kutatia |
| iv. | mstari | Nuile urapinga |
| v. | Pinsele | Niki chapingua |
| vi. | Barafu | Niile Buutuba choreo |

Kielelezo **6.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya katika swali hili. Mfano katika kipengele cha pili (ii) 'Mtahiniwa aliweza kuandika 'Msumeno' katika vifaa lkn katika matumizi hakuweza kuonesha matumizi ya Msumeno badala yake aliandika 'ni ule unachongwa'. Hii inaonesha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na uwelewa wa kutosha katika swali aliloulizwa.

Aidha, watahiniwa **2,549** sawa na asilimia **56.83** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya maana na dhana ya uchonjaji pamoj chokile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **6.2**

**Kielelzo kizuri 6.2**



a. Elezea maana ya kuchonga.

Kuchonga ni kazi ya sanaa ya kutengeneza maumbo mbalimbali kwa vitu rapu kama vile mawe, mbao nk.

b. Taja vifaa sita (6) vinavyohitajika wakati wa kuchonga pamoja na matumzi yake.

| Na. | KIFAA | MATUMIZI |
|---|---|---|
| i. | Nyundo | Inatumika kwa kugongea |
| ii. | Penseli. | Inatumika kwa kuchora. |
| iii. | Msumari | Inatumika kwa kugiia mbao |
| iv. | Vanish / rangi. | Inatumita kwa kupendezesha mbao |
| v. | Msasa. | Unatumika kwa kusafichia. |
| vi. | Mbao | Inatumika kwa kutengeneza vitu. |

Kielelezo **6.2** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alilifahamu vizuri swali aliloulizwa na alikuwa na uwelewa mzuri hivyo kupelekea kujibu swali kwa usahihi kama lilivyotaka.

### 3.2.3 Swali la 7: Ubunifu

Swali hili linatokana na mada ya 'Ubunifu', swali hili lilikuwa na vipengele viwili, kipengele (a, na b) kipengele ( a) kilikuwa na alama nne (4) na kipengele (b) kilikuwa na alama tano (5) na kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama tisa (9).

**Kipengele (a)**

Kipengele hiki kilmtaka mtahiniwa kutaja njia nne(4) za kiasili zinazotumika kuhifadhi chakula ili kisiharibike.

**Kipengele (b)**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kutaja vifaa vitano (5) vinavyotumika kuhifadhia chakula

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,442** sawa na asilimia **98.26** na watahiniwa **79 s**awa na asilimia **1.74** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 2c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,296 | 29.17 | 2,192 | 49.35 | 954 | 21.48 | 3,146 | 70.83 |

Takwimu za Jadweli nambari **2c** zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **21.48** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri kwa asilimia **70.83**

Aidha, watahiniwa **1,296** sawa na asilimia **29.17** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **7.1**.

**Kielelzo kibaya 7.1**


a. Taja njia nne (4) za kiasili zinazotumika kuhifadhi chakula ili kisiharibike.

1 Chakula utaka kisiharibike kitie ndani fu
2 Chakula ukitaka basi usikifunike
3 Chakula kiache kipate upepo
4 Chakula Ukitaka Kifunike kidonge


b. Taja vifaa vitano (5) vinavyotumika kuhifadhia chakula.

1 Bakuli la mfiniko
2 Bakuli la Hotipote
3 Bakuli la Ubati
4 Na vifaa friatuno
5 Bakuli la au mfiniko

Kielelezo **7.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya katika swali hili. Mfano katika kipengele (a) ‘Mtahiniwa aliweka maelezo badala ya kutaja njia za kiasili za kuhifadhia chakula kama ‘kutia chumvi’. Hii inaonesha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na uwelewa wa kutosha katika swali aliloulizwa

Aidha, watahiniwa **954** sawa na asilimia **21.48** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **7.2.**

**Kielelzo kizuri 7.2**


Taja njia nne (4) za kiasili zinazotumika kuhifadhi chakula ili kisiharibike.

Kuanika juani

Kupambia au kuchoma moto

Kukifunika

Kukitia kwenye friji

Taja vifaa vitano (5) vinavyotumika kuhifadhia chakula.

Friji

Sufuria

Ufunikio

Oveni au tanuri la moto

Kielelezo **7.2** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alilifahamu vizuri swali aliloulizwa na alikuwa na uwelewa mzuri hivyo kupelekea kujibu swali kwa usahihi.

### 3.2.4 Swali la 8: Kuogelea

Swali hili linatokana na mada ya ‘Kuogelea’, swali hili lilikuwa na vipengele viwili, kipengele (a, na b) kipengele ( a) kilikuwa na alama tatu (3) na kipengele (b) kilikuwa na alama sita (6) na kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama tisa (9).

**Kipengele a**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kueleza jinsi utakavyofundisha kanuni tatu (3) za kuogelea kwa ushindani.

**Kipengele b**

Na kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi mitindo mitatu (3) ya kuoglea

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,337** sawa na asilimia **95.93** na watahiniwa **184 s**awa na asilimia **4.07** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 2d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| – 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,352 | 54.23 | 1,371 | 31.61 | 614 | 14.16 | 1,985 | 45.77 |


Takwimu za Jadweli nambari **2d** zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **14.16** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **45.77**

Aidha, watahiniwa **2,352** sawa na asilimia **54.23** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **8.1**

**Kielelzo kibaya 8.1**


8. a. Bwana Mkude ametoka Morogoro na kuja visiwani Zanzibar kujifunza kuogelea kwa ushindani. Eleza jinsi utakavyomfundisha kanuni tatu (3) za kuogelea kwa ushindani.

Kuogelea bila ya kuwana wasiwasi
Kuogelea na Vifa vya Uogelea.
Kuogeleq na bila ya kuhofia Ushindi wa mwenzako



b. Kwa ufupi elezea mitindo mitatu (3) ya kuogelea.

Kuogelea na Vifaa mbalimbali ili kuweza kuogelea kwa Ushindani wa hali ya juu.
Kuweza kuwa na Uwezo mzuri wa kufuata kanuni za mchezo
kuwa na shauku ya kushinda na kuvaa zile Nguo zinazo takiwa kuogelea kama miwani ya kuoge lea, bukta na shati, Viatu,

Kielelezo **8.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya katika swali hili. Mfano katika kipengele (b) 'Mtahiniwa alitakiwa kuandika mitindo mitatu (3) ya kuogelea na aliandika 'kuogelea na vifaa, kuweza kuwa na uwezo mzuri, kuwa na shauku,' hili sio jawabu sahihi.

Aidha, watahiniwa **614** sawa na asilimia **14.16** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **8.2.**

**Kielelzo kizuri 8.2**



8. a. Bwana Mkude ametoka Morogoro na kuja visiwani Zanzibar kujifunza kuogelea kwa ushindani. Eleza jinsi utakavyomfundisha kanuni tatu (3) za kuogelea kwa ushindani.

i) Muogeleaji lazima ahitimu mafunzo uogeleaji kwa ushindani.
ii) Waogeleaji lazima wavae masafa na aina ya uogeleaji
iii) Bwawa la kuogelea liwe na ukubwa wa mita hamsini.

b. Kwa ufupi elezea mitindo mitatu (3) ya kuogelea.

i) kipepeo ni kuogelea kwa mikono inapepea kama kipepeo.
ii) kifua cha kifua
iii) Kistimia - ni hali ya kuogelea kwa mgongo mgongo.

Kielelezo **8.2** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alilifahamu swali vizuri na alikuwa na uwelewa wa kutosha hivyo kupelekea kujibu swali kwa usahihi.

### 3.2.5 Swali la 9: Afya katika Michezo

Swali hili linatokana na mada ya 'Afya katika Michezo', swali hili lilikuwa na vipengele vitatu (3), kipengele (a, b na c) kipengele ( a) kilikuwa na alama nne (4) na kipengele (b) kilikuwa na alama tatu (3) na kipengele (c) kilikuwa na alama mbili (2) hivyo kufanya swali hili kuwa na jumla ya alama tisa (9).

**Kipengele a**

Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya mlo kamili?

**Kipengele b**

Katika kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kutaja aina tatu (3) za vyakula.

**Kipengele c**

Mtahiniwa alitakiwa kuorodhesha madhumuni mawili (2) ya matumizi ya dawa

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **4,415** sawa na asilimia **97.65** na watahiniwa **106** sawa na asilimia **2.34** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 2e: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1774 | 40.19 | 1399 | 31.68 | 1242 | 28.13 | 2641 | 59.81 |

Takwimu za Jadweli nambari **2e** zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **28.13** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **59.81**

Aidha, watahiniwa **1,774** sawa na asilimia **40.19** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **9.1**

**Kielelzo kibaya 9.1**


9. a. Nini maana ya mlo kamili?

Mlo kamili ni mlo ambao mwanaadamu akila anakuwa yuko fiti na huweza kufanya kazi zake.

b. Taja aina tatu (3) za vyakula.

Mihogo

Ndizi

Majimbi

c. Orodhesha madhumuni mawili (2) ya matumizi ya dawa.


Kumfanya mtu kuwa yuko fiti

Kuondoa vidudu katika mwili.

Kielelezo **9.1** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alifanya vibaya katika swali hili. Mfano katika kipengele (a)'Mtahiniwa alieleza maana ya mlo kamili, '*Mlo kamili ni mlo ambao binaadamu akila anakuwa yuko fiti na huweza kufanya kazi zake*' hili silo jawabu sahihi la swali aliloulizwa.

Aidha, watahiniwa **1,242** sawa na asilimia **28.13** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **9.2**

**Kielelzo kizuri 9.2**


9. a. Nini maana ya mlo kamili?

mlo kamili ni mkusanyiko wa aina saba za vyakula kwa kiwango kinachokubalika na kwa wakati maalumu.

b. Taja aina tatu (3) za vyakula.

Protini

Vitamini

Mafuta

c. Orodhesha madhumuni mawili (2) ya matumizi ya dawa.

kinga

tiba

Kielelezo **9.2** ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri, hii inaonesha kuwa mtahiniwa alilifahamu swali vizuri na alikuwa na uwelewa wa kutosha hivyo kupelekea kujibu swali kwa usahihi.

### 3.3 SEHEMU C: Maswali ya Kuelezea

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu 10, 11 na 12, kila swali lilikuwa na alama ishirini (20) mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja tu kati ya maswali hayo.

#### 3.3.1 Swali la 10: Unyanyasaji wa Kijinsia

Swali hili linatokana na mada ya ‘Maigizo.

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuelezea njia nne (4) zitakazo punguza vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambavyo vimekuwa vikiongezeka kwa kasi katika jamii yetu.

Watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa ni **1,343** sawa na asilimia **29.71** na watahiniwa **3,178** **s**awa na asilimia **70.29** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| – 0-4 | | 4.5 - 12 | | 12.5 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 536 | 39.92 | 466 | 34.69 | 341 | 25.39 | 807 | 60.08 |

Takwimu za Jadweli nambari **3a** zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **25.39** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **60.08**

Aidha, watahiniwa **536** sawa na asilimia **39.92** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **10.1**


**Kielelezo 10.1 Kielelezo Kibaya**


10) i Kuondoa vitendo vyote ambavyo havinavyo ipunguza nchi yetu ya upendo.
ii) Achane kuwanyasa watoto ambao hawana wazazi wala
iii) Unyanyasaji wa kijinsia watoto wakifanyiwa wanaona hayo hata kutoka nje.
iv) Kuwanyanyasa maskini kwa kusaidia yo wao wanajiona matajiri.

Kielelezo **10.1** kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili, kwa mfano Mtahiniwa alijibu ila ameshindwa kuelezea matakwa ya swali husika hivyo mtahiniwa huyu aliandika athari za kufanyiwa vitendo vya kijinsia kwamfano kipengele cha tatu (iii) ‘ Unyanyasaji wa kijinsi wakifanyiwa watoto wanaona hay ahata kutoka nje’ badala ya kuandika njia zitakazopunguza vitendo hivyo. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali husika na pia alikuwa na uwelewa mdogo juu ya mada ya unyanyasaji wa kijinsia.

Aidha, watahiniwa **341** sawa na asilimia **25.39** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **10.2**

**Kielelzo kizuri 10.2**


10. Njia zitakazopunguza vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

1. Kutoa elimu juu ya unyanyasaji wa kijinsia. Ukitoa elimu vitendo hivyo vitapungua sana katika jamii kwa sababu mtu akitaka kufanya hivyo atakumbuka yale aliyoambiwa.

2. Kuhamasisha wanafunzi kufatana makundi kwa makundi. Wanafunzi wanaotoka shule ni vizuri wafatane kwa makundi kwa sababu akitokea mtu mbaya hawezi kuwadhuru

3. Kutoa taarifa polisi juu ya kufanyika kwa unyanyasaji wa kijinsia. Ukitoa taarifa vitendo vya ujambazi vitapungua sana kwa sababu mtu atahofia kufanya hivyo kukaa Jela.

4. Kuwapa elimu kundi linalotarajiwa kuingiya katika watu wanaofanya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia. Mtu akitoa elimu kwa watu hao vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia vinaweza kupungua katika jamii na ~~ekiepe~~ akihamasika kwa hilo aliloambiwa hawezi kufanya hivyo tena.

Kielelezo 10.2 ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili, na amejitahidi kuelezea kama swali lilivyotaka.

**3.3.2 Swali la 11: Afya katika Michezo**

Swali hili limetokana na mada ya ‘Madawa ya Kulevya’. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua madhara matano (5) yanayoweza kupatikana kwa kutumia dawa zisizokubalika.

Watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa ni **596** sawa na asilimia **13.18** na watahiniwa **3,925 s**awa na asilimia **86.82** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| – 0-4 | | 4.5 - 12 | | 12.5 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 276 | 46.31 | 192 | 32.22 | 128 | 21.47 | 320 | 53.69 |

Takwimu za Jadweli nambari **3b** zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **21.47** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambao umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **53.69**

Aidha, watahiniwa **276** sawa na asilimia **46.31** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **11.1**


**Kielelezo 11.1 Kielelezo Kibaya**


i. Kuzuiliwa kungia katika michezo
ii. Kuharibika kwa mifumo mbali mbali katika mwili
iii. Kutocheza kwa ufasaha
iv. Kufanya vitendo visivyokubalika katika michezo
v. Kuhujumu timu husika.

Kielelezo **11.1** kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili, mtahiniwa aliandika madhara ya matumizi ya madawa yasiyokubalika lakini hakuweka ufafanuzi wa madhara hayo kama swali lilivyotaka. Kwa mfano '*Katika kipengele cha tatu (iii)* mtahiniwa aliandika *'Kutocheza kwa ufasaha'* hivyo hapo inaonesha kuwa mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali husika.

Aidha, watahiniwa **128** sawa na asilimia **21.47** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu mzuri juu ya kile walichoulizwa kama inavyothibitisha katika kielelezo nambari **11.2**

**Kielelzo kizuri 11.2**


11
Dawa ni kitu chochote kiingiacho katika mwili na kubadilisha utendaji kazi wa mwili. Dawa zimegawanyika katika sehemu mbili katika michezo nazo ni dawa zinazokubalika katika michezo na dawa zisizokubalika katika michezo.


Vile vile dawa hutumika kama tiba na kinga. Kwa tiba dawa hutumika kutibu maradhi mbali mbali kama vile Malaria, ebola, kifua kikuu n.k. Kwa kinga dawa hutumika katika kujikinga na madhara au maradhi mbali mbali mfano kifua kikuu. Surua, pepo punda, tete kuwanga n.k.

Madhara matano (5) yanayoweza kutokea endapo wangetumia dawa zisizokubalika katika michezo ni kama yafuatayo:-

Kuzuiliwa kushiriki katika michezo. Mtumiaji anaetumia dawa zisizokubalika katika michezo huzuiliwa kushiriki michezo ni kwa sababu anaweza kufanya mambo ambayo hayaruhusiwi michezoni.

Dawa kumzoea mtumiaji
Mtu anaetumia dawa zisizokubalika katika michezo huenda zikamzoea na kushindwa kuzikataa na hali hii huweza kumpeleka madhara.

Kuharibika kwa uwezo wa kufikiri
Mtumiaji huweza ataharibika uwezo wake wa kufikiri kwa kutumia dawa zisizokubalika



katika michezo na kumpeleka ugonjwa wa akili
Kupungua kwa kiwango cha mchezaji
Mtumiaji anauwezekano mkubwa wa
kupungua kiwango cha kucheza na hali hii
itampelekea kutochaguliwa na kuwekwa nje.
Kupungua kwa utendaji kazi kwa mtumiaji
Mtumiaji anaweza kupungua utendaji wake wa
kazi na kumpelekea kuharibikiwa kwa mambo
yake kwa sababu dawa anazotumia humfanya
mtumiaji aregee.

Kielelezo **11.2** ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili, kwani aliweza kutaja madhara matumizi ya madawa yasiyokubalika lkn pia aliweza kuyatolea kama swali lilivyotaka.

### 3.3.3 Swali la 12: Ubunifu

Swali hili lilitokana na mada ya ‘‘Ubunifu’’. Swali lilimtaka mtahiniwa kuelezea hatua tano (5) anazoweza kuzifuata katika kutengeneza juisi ya parachichi.

Watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa ni **2,201** sawa na asilimia **48.68** na watahiniwa **2,320 s**awa na asilimia **51.32** hawakujibu swali husika.


**Jadweli nambari 3c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| – 0-4 | | 4.5 - 12 | | 12.5 - 20 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 228 | 10.36 | 901 | 40.93 | 1072 | 48.71 | 1973 | 89.64 |

Takwimu za Jadweli nambari **3c** zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa **48.71** upo katika kiwango cha ufaulu mzuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri kwa asilimia **89.64**

Aidha, watahiniwa **228** sawa na asilimia **10.36** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya swali lilivyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **12.1**

**Kielelezo kibaya 12.1**



Mahitaji
Sukari
Kisu
Bakuli
Aphi
Nakauzaliha
Hatua
Kutia maparachichi katika beseni la maji

Kielezo **12.1** kinaonesha karatasi ya mtahiniwa aliyefanya vibaya katika swali hili, mtahiniwa aliweka mahitaji ya utengenezaji wa juisi ya parachichi ambayo sio sahihi, kwa mfano aliandika ''*mahitajio: sukari,kisu, bakuli, arki, nakazalika.* na katika hatua, ameweka hatua moja tu, '' *Kutia maparachichi katika besi la maji''*. Hivyo inaonesha wazi kuwa mtahiniwa hakuwa na ufahamu wa kutosha juu swali hili. Kwani alitakiwa kuweka hatua sahihi za utengezaji wa juisi ya parachichi kwas usahihi pamja na hatua zake zote

Aidha, watahiniwa **1072** sawa na asilimia **48.71** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ufahamu wa kutosha juu ya swali walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari **12.2**

**Kielelezo kizuri 12.2**

Juisi ya Parachichi
Mahitaji ya juisi ya Parachichi
Parachichi , tangawizi, Sukari, ndimu,
Bakuli, mwiko na chujio, maji, kisu.
Hatua za kuandaa
1 kosha matunda pamoja na tangawizi
kwa maji safi
2 Menya tangawizi kwa kutumia kisu na
ukate vipande vidogo vidogo.
3 kata parachichi kwa kutumia kisu na
utowe nyama ya ndani
4 Tumia blenda kwa kusagia parachichi
na tangawizi
5 Tia kwenye bakuli na uchuje ili kuondoa
mabaki ya parachi na tangawi kisha na
utie sukari.

Kielelezo **12.2** ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili, kwani aliweza kutaja mahitaji ya kutengeneza juisi ya parachichi kwa usahihi na ameweza kueleza hatua za kutengeneza juisi hiyo kama swali lilivyoulizwa.

**4.0 HITIMISHO**

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali nane yalijibiwa vizuri na maswali manne yalijibiwa kwa kiwango cha wastani hakukuwa na swalai lililojibiwa vibaya.

Uchambuzi wa jumla unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walishindwa kupata ufaulu mzuri kutokana na ufahamu mdogo wa maswali husika katika mada mbalimbali zilizoulizwa, lakini pia ni pamoja na uwezo mdogo wa kujibu maswali hususan yale ya kuelezea.

Mwisho, taarifa hii ya kufaulu itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa somo hili la Sanaa, ubunifu na michezo kwa kiwango kizuri zaidi Inshaallah.

**5.0 MAPENDEKEZO**

- Walimu lazima wawahimize wanafunzi katika kufanya mazoezi ya kujibu maswali pamoja na kupitia masomo yao.
- Walimu wajitahid kutumia vitendo zaidi kwa mada ambazo zinazoweza kufundishwa kwa vitendo.
- Kuwe na mashindano ya kujielezea wanafunzi wenyewe na hata kutoa mada na kuwataka wanafunzi waelezee, hii itawasaidia sana katika kujibu maswali ya kuelezea kwani katika maswali ya kuelezea wanafunzi wengi hawakuyajibu inavyotakiwa na wengine hawakujibu kabisa.
- Kufanyike jitihada maalumu za kufundishwa wanafunzi kuandika kwani miandiko ya baadhi ya watahiniwa haifahamiki vizuri.
- Walimu wajitahidi zaidi kutoa kazi za vikundi na kufuatilia ushiriki wa kila mwanafunzi ili kuwasaidia wale wazito waweze kunyanyuliwa na wenzao.

**VIAMBATANISHO**

**KIAMBATANISHO NAMBARI 1**

**UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2023**

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | MAELEZO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Afya katika Michezo, Ubunifu, Ujasiriamali, Kuogolea na Sanaa za Lugha. | 3 | 97.65 | NZURI |
| 2 | Afya katika Michezo, Uchongaji, Huduma ya Kwanza katika Michezo, Sanaa za Lugha na Maigizo | 1 | 94.99 | NZURI |
| 3 | Ujasiriamali, Ubunifu, Uchongaji, Kuogolea, Huduma ya Kwanza katika Michezo. | 4 | 92.36 | NZURI |
| 4 | Afya katika Michezo | 11 | 89.64 | NZURI |
| 5 | Huduma ya Kwanza katika Michezo na Afya katika Michezo. | 2 | 87.60 | NZURI |
| 6 | Uchongaji | 6 | 85.70 | NZURI |
| 7 | Ubunifu | 7 | 70.83 | NZURI |
| 8 | Sanaa za Lugha. | 5 | 66.68 | NZURI |
| 9 | Afya katika Michezo | 9 | 60.80 | WASTANI |
| 10 | Kuogolea | 8 | 59.81 | WASTANI |
| 11 | Maigizo | 10 | 53.69 | WASTANI |
| 12 | Ubunifu | 12 | 45.77 | WASTANI |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2**

**UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2022**

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuogolea, Huduma ya Kwanza katika Michezo, Ubunifu, Afya katika Michezo, Ujasiriamali, Sanaa za Lugha. | 3 | 95.04 | NZURI |
| 2 | Kuogolea, Huduma ya Kwanza katika Michezo, Ubunifu, Afya katika Michezo, Ujasiriamali. | 1 | 87.63 | NZURI |
| 3 | Huduma ya Kwanza katika Michezo. | 2 | 74.56 | NZURI |
| 4 | Ujasiriamali. | 11 | 55.70 | MBAYA |
| 5 | Huduma ya Kwanza katika Michezo. | 10 | 41.30 | MBAYA |
| 6 | Ujasiriamali. | 7 | 40.89 | MBAYA |
| 7 | Kuogolea, Huduma ya Kwanza katika Michezo, Ubunifu, Afya katika Michezo. | 4 | 33.51 | WASTANI |
| 8 | Ubunifu. | 12 | 23.64 | WASTANI |
| 9 | Sanaa za Lugha. | 6 | 19.66 | MBAYA |
| 10 | Uchongaji. | 9 | 18.19 | MBAYA |
| 11 | Ujasiriamali, Ubunifu, Kuogolea. | 5 | 10.39 | MBAYA |
| 12 | Sanaa za Lugha. | 8 | 8.29 | MBAYA |